

Katiba ya Afrika kuhusu haki na ustawi wa mtoto

Kila mtoto ni sawa na ana haki sawa.” Haki” ni vipengee ambavyo kila mtoto anastahili kuwa navyo ama kuvifanya. Haki hutoa mwelekeo kuhusu yale yaliyo mazuri kwa watoto katika hali tofauti tofauti na kutufahamisha yale yaliyo ya muhimu ili kujinasua kutoka kwa madhara. Karibu kila taifa duniani limekubaliana na haki zilizo nukuliwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa (United Nations Convention), kuhusu haki za mtoto. unapokua, utaweza kufanya maamuzi yako kibinagsi, na pia kuwakilisha haki zako.



Nakala

- 1** Jirani yako sharti atambue sheria na uhuru wako. Jirani yako atazingatia hizi sheria ili kuepuka kufanya jambo lolote linaloenda kinyume na haki na uhuru wako!
- 2** Mtoto ni mtu ye yote aliye chini ya umri ya miaka 18.
- 3** Kila mtoto anaruhusiwa kufurahia hizi haki! Miaka, taifa, dini, jinsia ama maoni yako haiathiri uhuru wako.
- 4** Iwapo una maoni ya kusema, una uhuru wa kuyasema. Ni sharti watu wazima wasikize unayosema.
- 5** Una haki ya kua hai.
- 6** Una haki ya kua na jina na kutambuliwa na serikali.
- 7** Una uhuru wa kutoa maoni yako kama unaweza.
- 8** Una haki ya kutengeze ama kujiunga na kikundi ama klabu, bora isiwe na madhara kwa wengine.
- 9** Una haki ya kufikiri, kuamini na kuweka vitendoni chochote utakacho.
- 10** Una haki ya siri.
- 11** Una haki ya kujifunza, kuchunguza talanta yako na kutambua nini hukufurahisha zaidi. Serikali yako ni sharti itoe nafasi bora ya usawa ya masomo kwa wasichana, wanafunzi walio na vipaji na pia wanafunzi wasiobahatika. Mfumo wa elimu utasaidia kijifunza kuhusu utamaduni na maadili mazuri ya Afrika.
- 12** Una haki ya kucheza kwa uhuru.
- 13** Iwapo wewe ni mlemavu wa kiakili ama kimwili, una haki ya ulinzi maalum ili kusaidia kua mshiriki tendaji wa jamii na asiyetegemea.
- 14** Una haki ya afya ya kimwili, kiakili na kihisia. Pia una haki ya huduma ya afya, chakula bora, na maji safi na salama ya kunywa.
- 15** Unalindwa kutokana na kufanya kazi hatari ama inayoathiri kukua kwako, kwa namna yeyote.
- 16** Unalindwa kutokana na aina yoyote ya unyanyasaji na mateso.

17

Iwapo wewe ni mtoto na uvunje sheria, bado unalindwa kutokana na mateso au unyanyasaji.

18

Una haki ya ulinzi maalum unapoishi na familia yako.

19

Una haki ya kuishi na wazazi wako, na utatengwa na wao iwapo serikali inahitaji kulinda.

20

Wazazi wako au walezi ni sharti kila mara wakulinde na kutunza kwa namna yote bora iwezekanavyo..

21

Ni sharti Serikali kukomesha mazoea yaliyo na madhara kwako, kama vile ndoa za mapema kwa watoto.

22

Hamna aliye na haki ya kulazimu kuenda kushiriki vita kama mwanajeshi.

23

Iwapo wewe ni mkimbizi, una haki ya ulinzi na usaidizi wa kibinadamu.

24

Iwapo umetengwa na wazazi wako, unaweza pokea ulinzi maalum na kuwekwa katika huduma ya muda mfupi. Pia utapewa usaidizi wa kupata wazazi wako.

25

Ni sharti serikali kusaidia iwapo unaishi mahali ambapo hautunzwi kwa usawa.

26

Hamna anayeruhusiwa kutumia wewe kwa manufaa yake, kwa namna yeyote.

27

Umelindwa kutokana na kulazimishwa kutumia dawa za kulevyta.

28

Una haki ya kua huru kutokana na biashara za utumwa. Serikali yako itakulinda kutokana na kutekwa nyara ama kuuzwa kwa mtu yeyote.

29

Iwapo mwanamke ametuhumiwa kwa kuvunja sheria na ako na mimba ama ako na watoto wachanga, atapewa matibabu maalum.

30

Una wajibu wa kuheshimu familia yako, wakubwa wako na kuhifadi maadili na tamaduni za Afrika.